



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. SDC/S.10/52/243

Tarehe: 06/05/2024

TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI INATANGAZA NAFASI ZA AJIRA YA MKATABA KWA FANI ZIFUATAZO:-

- 1. DAKTARI DARAJA LA II- NAFASI TATU (03).**
 - a) SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe mwenye elimu ya kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI), aliyehitimu mafunzo ya Shahada ya Udakitari wa Tiba za Binadamu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na mwenye leseni hai inayotambuliwa na Baraza la Madaktari Tanganyika.

- b) KAZI NA MAJUKUMU YA DAKTARI DARAJA LA II:-**

- (i) Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali katika fani husika.
- (ii) Kupanga, kusimamia na kutathimini huduma katika wilaya au mikoa
- (iii) Kufundisha wanafunzi katika vyo vya afya vilivyo eneo lake la kazi
- (iv) Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa
- (v) Kutayarisha elimu ya kujiendeleza ya watumishi wa afya.
- (vi) Kufundisha na kuelekeza watumishi walio chini yake
- (vii) Kusimamia wafanyakazi walio chini yake
- (viii) Kubuni, kuendesha na kutathimini utafiti na kusambaza matokeo
- (ix) Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake
- (x) Kufanya kazi za Kitabibu zinazohusiana na maswala ya kisheria kama vile uchunguzi wa maiti
- (xi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi.

Atalipwa posho kulingana na Mwongozo wa Kufanya kazi kwa Njia ya Kujitolea kwa Watumishi wa Kada ya Afya uliotolewa na Wizara ya Afya mnamo Julai 2021.

2. MHUDUMU WA MOCHWARI - NAFASI MBILI (02)

a) SIFA ZA MWOMBAJI

Awe mwenye elimu ya kidato cha nne(IV) au kidato cha sita (VI), aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/ Cheti cha Uhudumu wa Mochwari katika chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

b). KAZI NA MAJUKUMU YA MHUDUMU WA MOCHWARI

- i. Kufanya usafi wa chumba cha kuhifadhia maiti.
- ii. Kutunza vifaa vya chumba cha maiti.
- iii. Kupokea, kuosha na kutunza maiti.
- iv. Kutunza kumbukumbu mbalimbali za utendaji kazi katika kitengo husika.
- v. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi.

Atalipwa posho kulingana na Mwongozo wa Kufanya kazi kwa Njia ya Kujitolea kwa Watumishi wa Kada ya Afya uliotolewa na Wizara ya Afya mnamo Julai 2021.

3. FUNDI SANIFU VIFAA TIBA – NAFASI MOJA (01)

a). SIFA ZA MWOMBAJI

Awe mwenye elimu ya kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI), aliyehitimu mafunzo ya Stashahada ya kawaida ya Ufundi wa Vifaa Tiba (Full Ordinary Diploma In Biomedical Engineering) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

b). KAZI NA MAJUKUMU:

- (i) Kufanya matengenezo ya vifaa tiba
- (ii) Kutunza kumbukumbu za kazi za kila siku.
- (iii) Kuagiza vifaa na vipuli vya kutengenezea vifaa Tiba ngazi ya wilaya.
- (iv) Kutunza vifaa Tiba na vipuli
- (v) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

Atalipwa posho kulingana na Mwongozo wa Kufanya kazi kwa Njia ya Kujitolea kwa Watumishi wa Kada ya Afya uliotolewa na Wizara ya Afya mnamo Julai 2021.

4. MSAIDIZI WA HESABU- NAFASI MBILI (02)

a). SIFA ZA MWOMBAJI

Awe mwenye elimu ya kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI), aliyehitimu mafunzo ya Cheti cha ATEC level II au “Foundation Level” kinachotolewa na “National Board of Accountants and Auditors”.

b). KAZI NA MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA HESABU

- i. Kuandika na kutunza “register” zinazohusu shughuli za uhasibu.
- ii. Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha.
- iii. Kutunza majalada yenye kumbukumbu za hesabu.
- iv. Kupeleka barua/nyaraka za uhasibu Benki.
- v. Kufanya usuluhisho wa masurufu, karadha, Hesabu za Benki na Amana.

Atalipwa posho kulingana na viwango vilivyowekwa na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti.

MASHARTI YA JUMLA:-

- i. Waombaji wote wawe na umri kati ya miaka 18 hadi 45.
- ii. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania.
- iii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani, namba za simu na majina mawili ya wadhamini pamoja na anuani zao na simu zao.
- iv. Waombaji wote wawe na kitambulisho ca taifa (NIDA) au namba ya kitambulisho.
- v. Waombaji wote waambatishe picha mbili za “passport size” za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma.
- vi. Watakaofaulu kuitwa kwenye usaili majina au orodha yao itawekwa kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya serengeti ambayo ni www.serengetidc.go.tz pamoja na kupigiwa simu.
- vii. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **20.05.2024 saa 09:30** alasiri.

Maombi yote yawaliloshwe masijala ya halmashauri kwa mkono au kutumwa kwa anuani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI,
S.L.P 176,
MUGUMU – SERENGETI.

Imetolewa Leo,
Tarehe **06.05.2024** na:-



Bwenda I. Bainga
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI
S.L.P 176
MUGUMU / SERENGETI